

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA

Simu Na: +255 26 2321607

Nukushi: +255 26 2322116

Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:-



Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

Kumb. Na. AH. 161/164/02/83

22 Desemba, 2021


Katibu Tawala wa Mkoa,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P. 5429,
DAR ES SALAAM.

Yah: **KIBALI CHA KUHAMISHA FEDHA ZA UJENZI WA MAJENGO YA DHARURA
(EMD) KWENDA HOSPITALI ZA MAJESHI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea barua yenye Kumb Na. TMMOH/U.63/01 ya tarehe 14 Desemba, 2021 kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke akiomba maelekezo ya fedha na utaratibu utakaotumika wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa jengo la dharura (EMD) kwa kuwa Hospitali inayotekeleza mradi wa ujenzi wa Jengo hilo inamilikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.
3. Mkoa wa Dar Es Salaam umepokea fedha za ujenzi wa majengo ya dharura katika Hospitali ya Mabwepande, Hospitali ya Polisi Kilwa Road na Hospitali ya Ukonga Chuo cha Maafisa Magereza. Aidha, Hospitali mbili (2) kati ya hizo zinamilikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.
4. Kwa barua hii, unaombwa umfahamishe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Jiji la Dar Es Salaam kuwa Kibali kimetolewa cha kuhamisha **Shilingi milioni mia sita (600,000,000.00)** kwenda Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya dharura katika Hospitali husika. Mkoa unakumbushwa kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika miradi hii.

Ninakushukuru kwa ushirikiano wako.


Dkt. Grace E. Magembe
KAIMU KATIBU MKUU